KISWAHILI KARATASI YA 2 – 1013/2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
MTIHANI WA MWIGO MACHI/APRILI 2018

**SIKATE TAMAA SHAIRI I**

1. i) Baadhi ya wanajamii hawa na utu / katili
   ii) Baadhi ya watu ni walafi, wachoyo, kupe n.k
   iii) Baadhi ya watu ni wanafiki
   iv) Alidhania pale walipofikia katika maisha ndipo starehe inapoanza, lakini ni kinyume
   v) Kwamba baadhi ya watu wana tabia ya wanyama Alama 5

b) i) Inkisari
   - yalo – wanomeza
   - medhani
   - zilo

ii) Tabdila
   - uweza (uwezo)

iii) Lahaja
   - hawano

iv) mazida
   - binadamu

v) Kufinyanga sarafu
   - ajabu hiyo nikupe

c) Nilipogeuka nyuma niliona maajabu/ watu waliokuwa na mwelekeo awali sasa wamepotoka au hawaoenekani au wametoweka (wako gizani). Walikuwa si binadamu tena bali wamekuwa waangamizi/ Hapa nikashangaa kama walikuwa chui wakufugwa.

d) Shimo – shida, tatizo, maagamizi
   Ukupe – utegemezi/ unyonyaji
   Thama – tena
   Tija – manufaa, faida

**SHAIRI 2 TAALUMA**

2a) - kurukia mambo si kuzuri
   - wanapozungumza wakubwa tusiingilie
   - kuingilia mazungumzo ya watu ni dalili ya kiburi
   - kukiwa na hatari, mtu asijiingize la sivyo atapigwa. Yoyote 3x1=alama 3

b) Mwenya nguvu mpishe alama 2

c) Lina mishororo mine katika kila ubeti
- lina vipande viwili, ukwapi na utao
- vina vya kati – ri na vya mwisho – e
- mizani minane katika kila kipande.

Shairi lina mizani 64 katika kila ubeti. Alama 4

d) i) Tarbia – mishororo mine katika kila ubeti
ii) mtiririko – vina vya kati na vya mwisho havibadiliki
iii) Manthawi – shairi lina vipane viwili ukwapi na utao
iv) Sakarani – shairi lina zaidi ya bahari moja Alama 4

e) i) Muyapate / mpokee
ii) Mwenye nguvu Alama 2

**TAMTHILIA K W WAMITILA – PANGO**

3a)
- maneno ya Ngwese
- anamwambia kauleni
- akio hotelini kwa kauleni
- amefika baada ya kupata habari kwamba vijana wakiongozwa na Katango, kibwana, kikubi na mbambekazi walikuwa humo hotelini mwa Kauleni
- ngwese anamkemea Kauleni kwa kuunga vijana mkono ila yeye alimsaidia kupata kiwanja. 4x1=alama 4

b) - Methali – Penye kuku wengi, usimwage mtama
- mdokezo 1x1=1

c)

-wanawake kuiheshimiwa – Katango anasema kuwa huu sio wakati wa wanawake kuolewa ili watiwe adabu na waume wao.

- Jamii yenye mshikamano na ambayo haisalitiani – sauti ya kizazi kipya inaita
- Wanawake kupata elimu sawasawa na wanaume kwani wao pia wanauwezo
- Vijana wanatetewa wachukue uongozi kutoka kwa wazee kwa wao pia wana uwezo
- Wanawake wanauwezo wa kushiriki katika siasa na uongozi sawa sawa na wanaume
- Jamii kupewa fursa ya kuwachagua viongozi ambao wanawajibika na waaminifu
- Utetezi juu ya jamii kutambua mchango wa vijana katika shughuli za uongozi
- Utetezi juu ya usawa katika jamii baina ya wnawake na wanaume
- Utetezi juu ya matumizi ya rasilimali ya jamii kwa usawa

- Utetezi juu ya dhuluma na unyanyasaji dhidi ya wanawake
- Kutupiliwa mbali kwa utamaduni uliopitwa na wakati kama upashanji wa tohara
- Viongozi wenye elimu na waadhilifu
- Wanajamii wasio na ubinafsi wa kutumia mali ya umma kwa ubadhirifu

10x1=10

**KITHAKA WA MBERIA – NATALA**

4. - Wakene kutaka kuhusiana kimapenzi na Natala – mke wa ndugu yake

- Jamaa ya Tango kumtarajia Natala arithiwe na wakene
- Chifu kutotaka mazishi yaendelee kabla ya kupewa hongo
- Mtunza ufuo anamtaka Natala kutoa hongo ili maiti atolewe
- Mtunza ufuo anataka kumnyanyasa Natala kimapenzi
- Wakene anataka kummjanganya Natala hati miliki ya shamba
- Ukoo unataka kumfukuza Natala na watoto wake kwenye nyumba ya Tango
- Wakene analewa ovyo ovyo na kukosa kuwajibikia jamii huku akimwacha Tila kuombaomba
- Watoto wa Natala wanadhulumiwa na mwanamke mmoja anayesema watakuwa vibawa
- Mama lime anamshawishi Natala aolewe na Wakene
- Mama lime anamwomba Wakene amtandike Natala
- Wezi wanaimba mavazi ya akina Tango
- Polisi wanachukua hongo ya shilingi hamsini ili wawachilie akina Tango
- Polisi wanawasingizia akina Tango kosa la kulewa
- Tila anamtusi Natala kwa kupewa chumvi kidogo
- Tila anamsingizia Natala kwamba anataka kuolewa na mumewe
- Polisi barabarani wanataka hongo
- Tango alifungwa kwa kosa ambalo hakufanya
- Tango na jammaa wengine walifungwa na hawakuruhusiwa kuwasiliana na jamaa zao
- Wakene kuota akiwa mbunge na kutoa hongo ya shilingi ishirini ishirini kwa wapiga kura
- Mama Lime kusema kuwa ndoa ya mke zaidi ya mmoja ina utulivu

15x1=15

**DUNIA MASHAKA MAKUU**

5a) Busara aliyotumia mwalimu Busar

- Kuwapa nafasi wanafunzi waeleze jambo lolote lililowatatiza pale shuleni. Dunia alieleleza kuwa mahusiano ya kimapenzi yaliwatatiza na akapendekeza madarasa ya wavulana na wasichana watenganishwe katika madarasa.
- Kusisitiza umuhimu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi na kuwaadhibu vikali wanafunzi walioonyesha dalili za kukosa nidhamu.
- Kuwashirikisha walimu katika kujadili swala la kutenga madarasa ya wavulana na wasichana ili kupunguza athari za mahusiano ya kimapenzi kati ya wanafunzi
- Kuwahusisha walimu katika hatua ya kupiga ili kufanyia uamuzi swala la kutenga madarasa ya wavulana na wasichana.  Waliounga mkono wakawa wengi kwa hivyo madarasa yakatenganishwa.
- Kutowahushisha wazazi katika swala la kutenganisha madarasa kwa vile aliona kuwa akiwahusisha wangeharibu mipango hiyo kwa kutoa maoni mengi tofauti na huenda uamuzi ambao ungefaa haungepatikana – C"Chui wengi hawamshiki tope."                    1x5=5

b) Matumizi ya nyimbo

- Baada ya kuzaliwa kwa dunia, Bi Nusura alimwimbia wimbo wa kumuongoa ili aache kulia baada ya kumpokea kutoka kwa Bi Mkunga.
- Wimbo ulioibwa na Bi Mkunga siku ya saba baada ya kuzaliwa, alipokuwa akipewa jina – wimbo wa kumtakia mema maishani
- Vilevile wimbo wa mkunga wa kumuongoa mtoto Dunia wa kumhimiza kula vizuri na kuwahimiza wazazi wamlee vyema.
- Wimbo wa ndege aliyemsaidia mwana mpika ndimu – ndege alimshauri achukue majani ya mti ayasugue vidondani ili vipone; vile vile ndge alimshauri kuwa akipatwa na njaa aikate ndimu vipane viwili aiombe impe wali, au chochote kile atakachotamani.
- Wimbo ulioibwa na mzee Mafusho alipokuwa akilima shambani mwake; maneno yake yakamtia moyo Yasibu alipokuwa msituni tayari kujiua kutokana na chuki ya babake.  Yasibu alibadilisha nia yake ya kujiua na kurudi nyumbani.
- Wimbo wa dunia alipokuwa gerezani akilivunja jabali.  Uchungu wa mateso aliyoyapata ukamkumbusha ushauri wote aliopewa ile siku alipokataa kuendelea na masomo ya shule ya upili.  Aliimba kuhusu mateso yaliyomfika akieleza kuwa alikuwa  tayari kurudi kwa wazazi wake wamamfae.

5x2=10

**MAISHA KITENDAWILI**

6a) Mukiadha

- Aliyesema maneno haya ni Papi
- Alikuwa akimwambia farida
- Walikuwa kibokoni wakijistarehesha kwa kunywa pombe
- Farida alikuwa ameenda kibokoni na mpenziye Kim
- Papi alijiunga nao baadaye na Kim akamjulisha kuwa Farida alikuwa mpenzi wake aliyekuwa akisoma katika chuo kikuu cha Mzalendo alama 5

b) - Waliendelea kunywa pombe hadi Kim akawa mlevi kupindukia hata akainamisha kichwa chini

- Kim alipoondoka ukumbini kwenda haja alikawia kurudi, naye Papi akaondoka kwenda na Farida byumbani kwake
- Alikaribishwa ndani ya ukumbi uliokuwa na kabati jeusi refu lenye nakshi
- Papi alijifungua kabati na Farida akaona kuwa ndani yake mlikuwa na maiti ya msichana
- Aliangizwa achukue mafuta na pamba ampake Yule maiti pole pole bila ya kughasi bali aweke tabasamu akiifanya kazi hiyo
- Alionywa kuwa asipofanya ghivyo angefanywa kuwa maiti pia
- Farida alijilazimisha kuifanya kazi hiyo kama alivyoamrishwa
- Hatimaye Papi alimwambia Farida aache kazi hiyo na akamlipa shilingi elfu moja.
- Papio alimrudisha Farida chuoni na akamuonya asimweleze yeyote kuhusu yale aliyoyaona nyumbani kwa Papi
- Papi alimpa Farida namba yake ya simu na kumwambia Farida ampigie simu wakati wowote iwapo angepata haja ya hela. 1x10= Alama 10

**SEHEMU YA C – MBINU ZA KUFUNDISHIA**

7a) Chanzo cha udhaifu / matatizo

1. Matamshi
   - Kudondosha – uruma badala ya huruma kupa
   - Kupachika – ndamu badala ya damu
   - Mapisharo ya vitamkwa – mdudu / mtutu
2. Kukosa ukakamavu, kuona haya
3. Athari ya lugha ya mama

4. Kukosa mazoezi mengi katika mafunzo hayo
5. Ujuzi haba wa kupima thamani na ubora wa yale wanayoyasikiliza kasha kuyaelewa/ hawana usikivu mwema
6. Kukosa msingi bora wa lugha fasaha
7. Mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili
8. Kukosa kielelezo bora cha kuiga kutokana na walimu, vyombo vya habari, wanasiasa na jamii kwa ujumla
9. Kukosa ubunifu
10. Kukosa utulivu na makini katika kuzingatia yasemwayo 10x1=10

b) Mafunzo

- Vitendawili - methali
- Matamshi - semi / nahau
- Matamshi - mafumbo

-Maamkuzi, adabu na heshima - taarifa kutoka vyombo vya habari/radio/runinga

- Vitanza ndimi - sauti tata
- Vichekesho - michezo mifupi ya kuigiza/maigizo
- Hadithi - tashubiha
- Mashairi - tanakali za sauti
- Nyimbo - hotuba fupi
- Majadiliano/mijadala Hoja zozote 5 =5

c) Mapendekezo / Njia za utatuzi

1. Awazoeze kutamka ipasavyo
2. Awape maneno mengi yenye sauti tata kwenye sentensi
3. Atumie nyenzo kila mara katika mafunzo na ziwe za kuvutia, kuimarisha aelewa
4. Kuhusisha wanafuzi wote katika mazoezi ya kusikiliza na kuongea
5. Kuwahimiza kutimia lugha ya Kiswahili kila mara ili kuondoa athari za lugha ya kwanza
6. Kuwa kielelezo bora yeye binafsi
7. Kualika watu mashuhuri katika lugha ya kiswhaili ilikuondoa mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili
8. Kuwapa mada za kiwango chao kama vile methali sahihi. Hadithi fupi zenye mvuto
9. Kuwashirikisha wanafuzi katika mashindano ya kuiga na kuigiza, kusimulia, kutega vitendawili n.k na watakaoshinda watuzwe
10. Kuwapa nafasi ya kujieleza na huwasilisha mawazo yao katika vipengele mbali mbali na kuwahimiza wanaposhindwa. Wakosolewe wakichekwa na wenzao, wanaowacheka wakomeshwe ili kustawisha ukakamavu wao.

11. Kurekebisha makosa ya matamshi, sarufi n.k yanapojitokeza katika mazungumzo darasani. Hoja zozote 5x1=5

8a)

- Kueleza maana ya nyakati, hali – ukanusho/na uyakinisho
- Kuwatajia viambishi vya nyakati
  Wakati – uliopita – kiambishi li
  Wakati – uliopo - " na
  Wakati – ujao - " ta
- Kuwatungia sentensi kudhuhurisha matumizi ya viambishi hivyo – li – na – ta
- Kuwapangia sentensi kudhuhurisha uyakinisho na ukanusho wa nyakati
  Li – na – ta
- Kuwapa nafasi kutunga sentensi wakitumia viambishi hivyo vya wakati – li-na-ta
- Kuwapa nafasi kudhuhirisha uyakinisho na ukanusho wa nyakati li-na-ta
- Kuwatajia viambishi vinavyobainisha hali na kuwaeleza namna vinavyotumika
- A – hali isiyodhuhurika
- Me – hali timilifu
- Hu – hali ya mazoea
- Po –
- Ki –
- Ka –
- Nge, ngali n.k
- Kuwatungia sentensi kudhihirisha hali hizo mbalimbali katika hali yakinishi
- Kutumia vifaa kama chati ya sentensi
- Maelekeze kuandika zoezi la kutunga sentensi katika umoja na wingi wakitumia nyakati na hali tofauti
- Kusahihisha na kurekebisha makosa ya sarufi, matamshi na majibu yasiyo sahihi. Hoja zozote 10x1=10

b) Ngeli ya u-zi huwa na makundi yafuatayo

i) Majina yanayoanza kwa nusu irabu

W katika umoja

| umoja | wingi |
|---|---|
| Wimbo | nyimbo |
| Waraka | nyaraka |
| Wayo | nyayo k.m |

Wimbo wake wapendeza
Nyimbo zao zapendeza

ii) Nomino zina zodondosha <u>u</u> kuonyesha wingi

| Umoja | wingi |
|---|---|
| Ukuta | kuta |
| Uteo | teo |
| Ufagio | fagio |
| Ukucha | kucha k.m |

Ufagio wake umepotea
Fagio zao zimepotea

iii) Nomino zinazodondosha <u>u</u> na kuchukua Ny

| Umoja | wingi |
|---|---|
| Uta | nyuta |
| Ufa | nyufa |
| Ua | njua |
| Uzi | nyuzi kwa mfano |

Uzi wake umekatika
Nyuzi zao zimekatika

iv) Nomino ambazo hudondosha u na kuchukua MB katika wingi

| Umoja | wingi |
|---|---|
| Ubeleko | mbeleko |
| Ubawa | mbawa |
| Ubinda | mbinda |
| Ubia | mbia |
| Ubavu | mbavu |

Ubavu wake umeumia
Mbavu zake/zao zimeumia

v) Nomino zinazochukua ND katika wingi

| Umoja | wingi |
| --- | --- |
| Ulimi | ndimi |
| Uwele | ndwele |
| Udvu | ndevu |

Ulimi wangu unauma
Ndimi zetu zinauma

Kila kikundi kilichotungiwa sentensi sahihi 5x2= 10
Umoja Alama 1
Wingi Alama 1 = Jumla 2

9a) Ufunzaji katiti
- Namna ya kutanguliza somo
- Namna ya kuendeleza somo/funzo
- Matumizi ya vifaa wakati wa kufunza
- Namna ya kuwatuza na kuwapongeza wanafunzi
- Namna ya kutumia mbinu tofauti tofauti za ufunzaji
- Namna ya kutumia mifano katika kielezea dhana Fulani
- Namna ya kueleza dhana kwa njia mwafaka
- Namna ya kuuliza wanafunzi maswali
- Namna ya kutumia lugha fasha, na sauti inayosikika
- Namna ya kutumia viziada lugha
- Namna ya kutathmini welewa wa wanafunzi
- Namna ya kutamatisha somo Hoja zozozte 10x1=10

b)

- Huondoa uchovu wa kutumia mbinu za kawaida za ufunzaji
- Wanafunzi huhusika vilivyo katika kipindi
- Mada hueleweka vyema
- Husaidia kudhibiti nidhamu kwa kuwashughulisha wanafunzi
- Huimarisha kumbukizi za mwanafunzi/wanafunzi
- Huwafanya wanafunzi kufuatilia mada kwa makini na tuo
- Huwachangamsha wanafunzi
- Huwafikirisha zaidi wakati wa ufunzaji na ujifunzaji
- Hutumika kurejelewa na wanafunzi na kuendelea kujifunza wenye hususani nyenzo kama chati / michoro inayoangikwa na kuachiwa darasani
- Hurahisisha maelezo na kufaulisha somo kwa urahisi

Hoja zozote 5x1=5